

*Kioo cha Lugha, Juz. 19(2), 2021, 18-38  
Jarida la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili  
Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.*

## **Ufasihi wa Matambiko: Uchunguzi wa Matambiko ya Wapangwa**

*Winne Stephen Mtega<sup>1</sup>*

### **Ikisiri**

Mojawapo ya sifa msingi zinazoipambanua fasihi ni matumizi ya lugha ya kisanaa (Mulokozi, 2017). Dhana ya ufasihi hujengwa kutokana na matumizi ya lugha teule, yenye ubunifu ndani yake na ambayo huweza kuvuta hisia za wasomaji au wasikilizaji wa kazi husika. Mpaka sasa kumekuwa na mjadala baina ya wanazuoni hususani wa fasihi kuhusu ufasihi wa tambiko. Mjadala huo umeibuka kwa lengo la kuhoji juu ya ufasihi uliopo kwenye tambiko na hata kudadisi ikiwa tambiko ni kipera cha fasihi au la (Samwel, 2013, 2015; Mulokozi, 2017). Samwel (2013) anatoa mtazamo wake kwa kueleza kuwa kinachochukuliwa kuwa ni fasihi katika tambiko ni maneno, yaani lugha ya kisanaa iliyotumika, manuizo pamoja na nyimbo na si matendo matupu yasiyo na maneno. Ufafanuzi wake ni muhimu japo hautoi ithibati yoyote inayooonesha udhihirikaji wa ufasihi huo. Kutokana na jambo hili kutokuwa wazi, makala hii imechunguza ufasihi wa tambiko na mifano imetolewa kutoka katika matambiko ya Wapangwa. Katika kufanikisha hilo, Nadharia ya Utendaji imetumika huku mawazo yake makuu yakisaidia kubainisha viashiria mbalimbali vya kifasihi vilivyojitokeza katika utendaji wa tambiko. Data za mjadala huu zilipatikana uwandani kuititia njia ya mahojiano na majadiliano ya kwenye vikundi ambayo yalifanyika baada ya kumaliza tukio la utambikaji. Makala hii ilibaini vipengele kadhaa vya kifasihi vilivyojitokeza katika matambiko ya Wapangwa. Baadhi ya vipengele hivyo ni matumizi ya mbinu za kishairi, takririni, tabano, nyimbo na lugha ya piche. Ujitokezaji wa vipengele hivyo vya kifasihi unadhihirisha ufasihi uliopo katika matambiko na kuyafanya yakidhi kuwa moja ya kipera cha fasihi simulizi.

### **1.0 Utangulizi**

Dhana ya tambiko imejadiliwa na wataalamu mbalimbali kama vile Swantz (1970), Hornby (1998) na Samwel (2013, 2015), kwa kuwataja baadhi. Wataalamu hao wamefasili na kuifafanua dhana ya tambiko kwa mitazamo tofauti. Swantz (1970)

---

<sup>1</sup> Mhadhiri Msaidizi, Idara ya Lugha na Fasihi, Kitivo cha Insia na Sayansi ya Jamii, Chuo Kishiriki cha Elimu Mkwawa, Iringa, Tanzania. Baruapepe: Mtegawinnie19@gmail.com

anaeleza kuwa tambiko ni alama ya mfumo na itikadi ya jamii husika. Anaongeza kuwa kuna aina mbalimbali za matambiko ambazo hujumuisha matambiko yanayohusu maisha, imani na roho pamoja na matibabu. Hii ina maana kwamba ijapokuwa kumekuwapo na nyanja nyingi za mabadiliko ya njia mbalimbali za kiutamaduni na za kijamii, bado kila jamii imekuwa na upekee fulani katika kudumisha masuala ya mila, imani na itikadi. Akiongeza katika hili, Hornby (1998) anaeleza kuwa tambiko ni itikadi ya jamii ambayo hufanyika katika kipindi na muda maalumu kama sehemu ya dini au sherehe. Utaratibu wa utendaji wa matambiko huwa ni wa namna moja kwa wakati wote ambapo tendo hilo linafanyika. Taratibu hizo huweza kuwa sawa au la kutoka jamii moja na nyingine. Mawazo haya yanaonesha kuwa tambiko ni utaratibu ambao unaweza ukajiegemeza katika misingi ya dini au likahusiana na sherehe mbalimbali za kijadi zinazopatikana katika jamii husika.

Tafiti nyingi zimefanyika kuhusu matambiko katika jamii na fasihi kwa ujumla. Tukitazama tafiti hizo tunaona nyingi zimejikita kuchunguza aina za matambiko, dhima zake, dhima za nyimbo za tambiko na taswira zinazopatikana katika nyimbo za tambiko; kwa kutaja baadhi (taz. Wilson, 1957; Dundas, 1968; Swantz, 1970; Mwakasaka, 1977; Mohamed, 2009; Mwasaka, 2012 na Hassan, 2013). Mbali na tafiti hizo kuhusu matambiko, bado kumekuwa na mijadala ambao haupo wazi kuhusu ufasihisi uliopo katika matambiko. Hali hiyo imesababisha baadhi ya wanataaluma kuhoji ikiwa matambiko ni kipera kimojawapo cha fasihi au la. Kutokuwapo kwa uwazi wa mijadala hiyo kuhusu ufasihisi uliopo katika matambiko kumewanyima uhuru watafiti na wanataaluma wengi hususani katika uga wa fasihi kuzidi kufanya tafiti kuhusu matambiko. Kwa mantiki hii ni kwamba tafiti nyingi zilizofanyika kuhusu matambiko hazijaweza kutoa ithibati toshelevu juu ya ufasihisi wa matambiko na udhihirikaji wake. Kabla hatujaendelea ni muhimu tutazame japo kwa ufupi kuhusu mijadala huo.

Kumekuwa na mikinzano katika kutolea ufanuzi ufasihisi uliopo katika kipera cha miviga<sup>2</sup> ikiwa ni pamoja na vipera vyake na kuelezwa kuwa baadhi ya mambo yanayotendeka katika miviga, na tambiko likiwamo, si fasihi bali huweza kuwa sanaa nyinginezo (taz. Mulokozi, 1996 na 2017; Samwel, 2013a, 2013b, 2015). Katika kufafanua hilo, Samwel (2013, 2015) anabainisha juu ya ufasihisi uliopo katika miviga na vipera vyake kwa kueleza kuwa kinachochukuliwa kuwa fasihi katika miviga ni matini zenye ufasihisi ndani yake na si matendo yasiyo na maneno. Kwa mfano, katika tambiko maneno, manuizo na nyimbo zinazoambatana na tukio husika ndiyo hukidhi sifa ya kuwa fasihi simulizi lakini si matendo yanayotendwa pasipo maneno. Kinachobainika hapa ni kwamba matumizi ya lugha teule na ya kisanaa

---

<sup>2</sup> Ngure (2003:69) anasema miviga ni sherehe au ibada ambazo huwa zinifuata utaratibu fulani wa kisanaa za maonyesho au fasihi simulizi. Mfano, kuna miviga ya kumpa mtoto jina, harusi, mazishi, matambiko, unyago na jando. Katika shughuli hizi, watu hufanya vitendo vyta kisanaa kama vile uchezaji ngoma, uimbaji, upigaji muziki, utongoaji mashairi – ukiambatana na matendo ya mwili na matumizi ya lugha.

ndiyo msingi wa kazi za fasihi, ijapokuwa bado maelezo hayo hayatoi ithibati yoyote juu ya udhihirikaji wa matumizi ya lugha hiyo teule katika matambiko.

Sambamba na hilo, Samwel (2015) anaongeza kuwa licha ya fasihi simulizi kuwa na tanzu nyingi, mojawapo ya tanzu zake ni drama simulizi ambayo pia huitwa maigizo au michezo ya kuigiza. Hapa anazungumzia maigizo kama yale ya jadi ya Kiafrika ambayo huambatana na ngoma, utambaji hadithi, sherehe za kiutamaduni kama vile jando, harusi, matambiko na matanga. Halikadhalika, Mulokozi (2017) anajadili kuhusu utanze wa maigizo na kudai kuwa kipera kimojawapo cha maigizo ni maigizo ya mivigani ambayo huambatana na matendo matukufu ya kimila. Kwa mfano, unyago, ibada, tambiko na sherehe kuu za kimila na kidini. Sherehe kuu za jamii kama vile kuzaliwa kwa mtoto, msiba, kuanua matanga, sherehe za kidini huwa na sanaa za maonesho ambazo huambatana na maigizo na miviga yenye kuakisi visasili vya jamii au taifa. Maelezo ya wataalamu hawa yanatubainishia kuwa matambiko ni kipera cha fasihi ambacho hupatikana katika drama simulizi na kinahusisha sifa muhimu za fasihi simulizi<sup>3</sup> ijapokuwa jambo hili halipambanuliwi kwa uwazi. Mbali na ufanuzi wa Mulokozi, jambo muhimu tunaloliona hapa ni kwamba maandiko hayo yanagusia tu suala hili pasipo kutoa ithibati yoyote kuhusu udhihirikaji wa ufasihi huo. Kutokuwapo kwa ithibati yoyote kunaleta ukakasi kwa wanataluma hasa kwa kutoonesha msimamo wao kuhusu ufasihi uliopo katika matambiko. Kutokana na utata huo, makala hii imechunguza ufasihi unaopatikana katika matambiko huku msimamo wake ukiegemezwa katika fikra kwamba msingi wa fasihi uko katika lugha teule na ya kisanaa ambao ndiyo hutumika kuwasilisha ujumbe kwa jamii iliyosudiwa. Kwa mantiki hiyo, makala hii inafafanua ufasihi uliopo katika matambiko ya Wapangwa na uchambuzi wake unajiegemeza katika maneno na lugha ya kisanaa inayotumika kuwasilisha matambiko husika.

## 2.0 Ukusanyaji wa Data

Data zilizotumika katika makala hii zilipatikana kutokana na utafiti uliofanyika uwandani. Maeneo yaliyohusika katika ukusanyaji wa data hizo ni kata ya Mlangali na Madope zinazopatikana katika wilaya ya Ludewa, mkoa wa Njombe. Maeneo hayo yaliteuliwa kwa kuwa wanapatikana Wapangwa asilia, hakuna mwingiliano mkubwa na makabila mengine na ni maeneo ambayo bado yanaendeleza utendaji wa matambiko. Katika kufanikisha mchakato wa ukusanyaji wa data, mtafiti alitumia mbini ya mahojiano na majadiliano ya kwenye vikundi. Hivyo, maswali ya mwongozo yaliandaliwa na kutumika kufanya mahojiano ya moja kwa moja na viongozi wa koo ambao ndio viongozi wa matambiko pamoja na wazee wenye hekima na uzoefu na mambo fungamani yanayohusiana na matambiko. Mathalani, koo nne ziliteuliwa na kutumika kama chanzo cha data za utafiti kulingana na data zilizohitajika. Baada ya kukamilisha mahojiano na viongozi wa tambiko, njia ya majadiliano katika vikundi iliyohusisha wazee ambao walihusika katika shughuli za

---

<sup>3</sup> Fasihi simulizi huwasilishwa kwa njia ya mazungumzo ya mdomo, huhusisha utendaji wa wahusika, uhai wa hadhira, uwapo wa tukio yaani, fani inayotendwa, wakati na mahali pa kutendea tukio husika kwa kutaja baadhi (Ngure, 2003; Mulokozi, 2017).

tambiko ilitumika. Majadiliano haya yalifanyika baada ya kumaliza tukio la utambikaji na kufika nyumbani kwa mwenye tambiko ili kuendelea na taratibu zingine ikiwa ni pamoja uimbaji wa nyimbo za kukamilisha tambiko na uchezaji wa ngoma. Kupitia njia hizo mtafiti alishuhudia mambo mbalimbali ambayo yalichochea majadiliano na hatimaye kufanikisha ukusanyaji taarifa muhimu zilizohitajika.

### **3.0 Nadharia ya Uchambuzi wa Data**

Katika kufanikisha malengo ya utafiti huu, Nadharia ya Utendaji imetumika. Nadharia hii inaelezea mbinu mojawapo ya mawasiliano inayohusisha uwajibikaji wa fanani kwa hadhira katika kazi za fasihi. Mbinu hiyo huhusisha matumizi ya lugha na namna ya kuzungumza. Nadharia hii imechota maarifa yake kutoka katika taaluma mbalimbali kama vile anthropolojia, isimu na fasihi (Bauman, 1975). Miongoni mwa waasisi wa nadharia hii ni Dan-Ben-Amos (1972) akiwa ni miongoni mwa waanzilishi wa sanaa ya jadi katika mkabala wa utendaji na baadaye nadharia hii iliendelezwa na Victor Turner (1982), Wallace Bacon (1984) pamoja na Richard Schechner (1985; 2013). Mhimili mkuu wa nadharia hii umejengwa katika kuwapo kwa viashiria vya kiutendaji vya kifasihi simulizi. Viashiria hivyo ndivyo vilivyotumika kufanikisha ubainishaji wa vipengele vya fasihi simulizi vilivyojiteza katika matambiko na kudhihirisha kuwa tambiko haliwezi kukamilika pasi kutumia vipengele vya kifasihi ambavyo ndivyo hulipa maana.

Kwa mfano, akielezea kuhusu utendaji katika fasihi simulizi, Bauman (1975) anataja viashiria vya utendaji wa kifasihi simulizi ambavyo hutumika kama mihimili inayoongoza nadharia hii kuwa ni pamoja na: matumizi ya lugha ya kipekee inayoashiria kikundi au utanze fulani kama vile matumizi ya lugha ya kisanaa. Kwa mfano, katika matambiko lugha inayotumika huwa na ubunifu ndani yake. Ubunifu huo hujidhihirisha wanapoanza kutoa salamu kwa wahenga kwa kusema, “Hodi! Hodi! Enyi mababu, mababu mliotukuka...”. Pili, kuwapo kwa hadhira. Kwa mfano, katika utendaji wa matambiko hadhira hujidhihirisha kupitia uwapo wa wahusika amba ni dhahania. Wahusika hao dhahania ni kama vile Mungu, miungu, wahenga, mahoka na mizimu. Wahusika hawa hawajidhihirishi katika hali ya kimwili bali huwapo katika fikra za fanani ama watendaji na huaminika kuwa wapo, wanaona, wanaskia na wanajibu maombi. Tatu, kuwapo kwa fomula maalumu ambazo huzingatiwa wakati wa utendaji. Kwa mfano, katika matambiko ya Wapangwa tumebaini kuwapo kwa mianzo na miisho ya kifomula ambayo hujidhihirisha pale kiongozi wa tambiko anapoanza kwa kubisha hodi mara tatu, kisha hurudia mara moja na kuwataja wahenga na mababu kwa majina yao. Nne, kuwapo kwa matumizi ya lugha ya picha au ya kisanaa. Tambiko huhusisha matumizi ya lugha za picha ambazo viashiria vyake hufungamana na tukio pamoja na jamii husika. Tano, kuwapo kwa mbinu rasmi za kielimu-mitindo kama vile matumizi ya takrir, urari wa vina pamoja na uimbikaji. Kanuni hizi zinamfanya mtu atambue kuwa ushairi na nyimbo ni mojawapo ya tanzu muhimu zinazotumika kukamilisha utendaji wa matambiko.

Sita, kunakuwa na uzungumzaji maalumu amba hauendani na ule wa mazungumzo ya kawaida. Uzungumzaji huo huhusisha matumizi ya sauti ya kughani, yaani iliyo kati ya kuimba na kuzungumza. Aina hiyo ya uzungumzaji huashiria

kwamba fanani anaingia kwenye utendaji wa utanzu fulani na huwa ni kitambulisho cha utanzu huo. Saba, kuwapo kwa maneno yanayorejelea utamaduni na jadi fulani. Kwa mfano, utendaji wa tambiko huhusisha uteuzi makini wa maneno ambayo kwayo hutambulisha tukio na kufungamana na utendaji wa tukio hilo. Kutokana na ufungamanifu huo, matumizi ya maneno kama wahenga, mizimu, mahoka, mababu watukufu yanapotajwa katika utendaji wa tambiko huashiria utamaduni wa jamii husika. Kimsingi, viashira hivi ndivyo vimekuwa chachu katika kufanikisha utambuzi wa vipengele vya kifasihi vinavyojitokeza katika matambiko na kudhihirisha ufasihhi wake.

#### **4.0 Historia Fupi kuhusu Jamii ya Wapangwa**

Wapangwa ni jamii ya watu wanaishi katika milima ya Livingstone karibu na Pwani ya Mashariki ya Ziwa Nyasa, hasa katika maeneo ya Madunda, Mawengi, Mlangali, Masimbwe, Mkiu, Madilu, Madope na Lupanga katika wilaya ya Ludewa, mkoa wa Njombe. Maeneo hayo yapo katika Ukanda wa Nyanda za Juu Kusini mwa Tanzania. Wapangwa huishi katika koo na masuala yote yanayohusiana na mila na tamaduni zao hufanyika katika utaratibu maalumu kwa kila ukoo (Stephen, 2007). Aidha, inaelezwa kuwa chanzo cha wao kuishi katika koo ni vita (Barndon, 2004). Kutokana na takwimu za Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2012, wilaya ya Ludewa ina watu 152,285 ambapo 72,968 ni wanaume na 79,318 ni wanawake. Akieleza juu ya upekee wa jamii ya Wapangwa, Barndon (2004) anadai kuwa tangu kale shughuli zao za kiuchumi ziliambatana na matumizi ya nguvu za kimiujiza, yaani uganga na sihiri, utoaji sadaka na shukrani kwa mizimu. Wapangwa walihusianisha shughuli hizo na ibada za kijadi wakiamini kwamba matambiko ndio njia pekee ya kuwapa nguvu na uwezo wa kufanikisha shughuli zao.


#### **5.0 Muktadha wa Utendaji katika Matambiko ya Wapangwa**

Muktadha wa utendaji wa matambiko katika jamii ya Wapangwa huhusisha mambo kadhaa kama vile aina za matambiko zinazopatikana katika jamii hiyo, wahuksika wa tambiko, mazingira ya kiutendaji na muundo wa tambiko. Katika jamii ya Wapangwa kuna aina mbalimbali za matambiko ambayo hufanyika kutegemea na uhitaji na malengo yaliyokusudiwa. Kwa mfano, kuna tambiko la uzazi ambalo hujidhihirisha kwa namna mbili. Kwanza, ni tambiko la uzazi kwa wale waliokosa kabisa kupata uzao. Pili, kupatikana kwa mtoto wa kiume ambaye huamini ndiye anayeendeleza uzao na kufanikisha kuukamilisha ulimwengu. Kuna tambiko la kuondoa mikosi, yaani mkosi wa kutokuolewa, kutokua, kuzalia nyumbani, vifo vya ajabu na vile vinavyotokea ghafla. Matambiko mengine ni kama tambiko la kutoa shukrani, kumhamisha marehemu na tambiko la kuanza msimu mpya wa kupanda mazao shambani.

Matambiko haya hufanyika katika koo, yaani kila ukoo una utaratibu wake wa kufanya tambiko na hii ndiyo sababu kuna viongozi wa koo, mila au matambiko ambao huratibu kanuni na taratibu zote za matambiko kulingana na miiko husika pamoja na mila fungamani za Wapangwa. Kitendo cha kila ukoo kufanya matambiko hakiwatofautishi kwani Wapangwa kama jamii moja wana mila na taratibu ambazo

kwayo zinawaunganisha. Kwa upande wa wahusika, matambiko ya wapangwa huhusisha wanaukoo pekee ambao tayari wamekwishafanyiwa mila na matambiko ya awali ya kuwatambulisha kwa wahenga kama sehemu ya ukoo husika. Hivyo, ikiwa mmoja hana sifa za ushiriki basi ni lazima afanyiwe taratibu za kimila ambazo zitasaidia kumwepusha na matatizo yanayoweza kujitokeza endapo atashiriki.

Kuhusu muundo wa uwasilishaji wa maombi tumbaini kuwa matambiko ya Wapangwa hifuata mfuatano maalumu uliopo katika ngazi kulingana na nguvu za kiutendaji. Mfuatano huo huanza na Mungu mkuu ambaye huaminiwa kuwa ndiye mwenye nguvu kuu katika kukamilisha maisha na ulimwengu; akifuatiwa na wawakilishi ambao huwa ni wahenga, yaani mababu waliokufa zamani. Baada ya wahenga hifuata viongozi wa koo, mila au tambiko na kisha ni wanaukoo wengine. Muundo huo unaonesha kuwa ili uweze kujibiwa maombi ni lazima uzingatie ngazi husika ambapo mwombaji hupaswa kueleza matatizo yake kwa kiongozi wa ukoo. Kiongozi huyo hupanga taratibu zote zinazopaswa kufuatwa ili kufanikisha mawasiliano na wahenga, hususani kuomba msaada juu ya mambo mbalimbali. Wahenga hupokea maombi na kuyafanya kazi. Maombi ambayo yapo nje ya uwezo wao huyawasilisha kwa Mungu mkuu. Tafsiri yake ni kwamba ufanyakaji kazi wa mfumo huo hutegemea mgawanyo wa kimajukumu ambao umefungwa katika uwezo na nguvu kulingana na daraja husika. Jambo muhimu ni kwamba hadhira inayopambanua nguvu hizo ipo akilini mwa watendaji na udhihirikaji wa utendaji wake hujipambanua kuititia namna maombi yanavyowasilishwa. Watendaji huamini kuwa hawawezi kuifikia nguvu kuu kabla ya kuwaomba wahenga ambao inaaminika ndio waliopewa mamlaka na nguvu za kuongoza maisha ya waliohai. Hivyo, maombi huwasilishwa kwa wahenga kisha huwaomba wahenga wawasadie kuomba kwa Mungu mkuu. Baada ya kufanya tambiko watambikaji huenda katika eneo walilotambikia ili kuangalia ikiwa sadaka walizopeleka zimechukuliwa. Kutozikuta sadaka hizo ambazo ni unga, pombe na nyama ni ishara kwamba wahenga wamepokea maombi yao na wapo tayari kuwasaidia na kuwaombea kwa Mungu mkuu. Mfuatano darajia wa nguvu za kiutendaji na muundo wa tambiko la Wapangwa unajidhihirisha katika Kielelezo Na. 1 kifuatacho:



**Kielelezo Na. 1: Muundo wa uwasilishaji wa matambiko ya Wapangwa**

## 6.0 Ufasihi katika Matambiko ya Wapangwa

Sehemu hii inabainisha na kufafanua ufasihi unaojitokeza katika matambiko ya Wapangwa. Katika kufanikisha hilo, hoja mbalimbali zimefanuliwa na mifano inayodhihirisha ufasihi huo imetolewa kutoka katika data msingi ambayo ni matambiko ya Wapangwa. Aidha, aina mbalimbali za matambiko zinazopatikana katika jamii ya Wapangwa zimetumika kama moja ya ithibati muhimu. Baadhi ya vipengele muhimu vya kifasihi vinavyojitokeza katika matambiko na kujadiliwa katika sehemu hii ni: matumizi ya lugha ya kisanaa ambayo ndiyo nyenzo kuu ya fasihi, matumizi ya nyimbo zinazoambatana na tambiko husika, utambaji wa fanani katika uwasilishaji wa maudhui kwa hadhira iliyokusudiwa; hapa kinachozingatiwa ni ule ushairi ambao fanani mkuu ambaye ndiye kiongozi wa tambiko hughani wakati wa uwasilishaji wa tambiko. Vipengele vingine ni uhusiano baina ya fanani na hadhira wakati wa uimbaji wa nyimbo za tambiko, na mbinu mbalimbali za kisanaa zinazotumika katika utendaji wa matambiko. Baadhi ya mbinu hizo ni matumizi ya takririni, lugha ya picha, matumizi ya balagha, mafumbo pamoja na matumizi ya sauti ya ughani katika kuwasilisha ujumbe kwa hadhira. Ufafanuzi huu utamsaidia msomaji wa makala hii kufahamu kwa kina vipengele vya kifasihi vinavyotumika katika matambiko na kudhihirisha ufasihi wa utanzu huo.

### 6.1 Matumizi ya Mbinu ya Kishairi

Mbinu za kishairi huwa na upekee wa kimatumizi ukilinganisha na kazi zingine za fasihi. Upekee huo unajidhihirisha katika uteuzi wa lugha ya kisanaa, matumizi ya muundo na mtindo huru ambao huhusisha matumizi ya sauti na sentensi fupifupi ambazo hazina urari wa vina na mizani, bali huwa zile zinazoweza kuimbika. Matambiko hutumia mbinu za kishairi ili kuwasilisha ujumbe uliokusudiwa. Mbinu hizo zinajidhihirisha katika Data Na. 1 kama ifuatavyo:

(1)

<i>Iliteghelo ilyaghuhecha imikosi ya lifwa</i>	<b>Tambiko la kuondoa mikosi (vifo)</b>
<p>1. <i>Hodi! Hod! Hod!</i></p> <p>2. <i>Nyeva hodi! Nyevakughu hodi</i></p> <p>3. <i>Hodi vanguluvi vetu yemuvele pa-sapo</i></p> <p>4. <i>Nyevakughu yemwitama isighu jchonda</i></p> <p>5. <i>Twichile twevana venyo</i></p> <p>6. <i>Tuletile imola jchetu</i></p> <p>7. <i>Twinyiligha mutupulighile nughutupyanila</i></p> <p>8. <i>Twinyiligha mututangagke nughutunyilighila</i></p> <p>9. <i>Twichile ghuvajchovela imola jhetu</i></p> <p>10. <i>Imola jchetulinacho ngomi</i></p> <p>11. <i>Sitwiwesa ughuhecha twinyiligha mututange</i></p> <p>12. <i>Inumbula chingina ghumaligha</i></p> <p>13. <i>Avana vetu vifwa ghilo</i></p> <p>14. <i>Ifwa iyi siyielewegha twilemwa naghujchova</i></p> <p>15. <i>Ngenyile namapanga pakilo</i></p> <p>16. <i>Tupoghile anywe isumu</i></p> <p>17. <i>Ifwa iyi siyalepwe paghatali</i></p> <p>18. <i>Tughivucha ghulighighi ughwe?</i></p> <p>19. <i>Twinyiligha mwivuchagke nayunye vayetu ughwe mututange imola ichi chisile nachileghaghe ughugomoghela ghangi</i></p> <p>20. <i>Tughavanyiligha muvalindaghe avana ava</i></p> <p>21. <i>Twinyiligha mutupyanilaghe nughutunyilighila ghwa vana vetu vakulagke vunofu vasomaghe valeghaghe ughwingila mumalanga ghaghwenivala ghuno</i></p> <p>22. <i>Tuvaletye uvughimbi, uvutine ninyama iyi</i></p> <p>23. <i>Mulichaghe nyevonda mututangagke twendelelaghe ughuva nulukelo pamwinga</i></p>	<p>1. Hodi! Hod! Hod!</p> <p>2. Jamani hodi! Mababu zetu hodi</p> <p>3. Hod! miungu yetu mliopo hapo chini</p> <p>4. Mababu mnaoishi milele</p> <p>5. Tumeuja sisi watoto wenu</p> <p>6. Tumeleta matatizo yetu</p> <p>7. Tunaomba mtusikilize na kutuhurumia</p> <p>8. Tunaomba mtusaidie na katuombea</p> <p>9. Tumeuja kuwaeleza shida zetu</p> <p>10. Matatizo yanayotukabiri ni makubwa</p> <p>11. Hatuwezi kuyatatua pasipo msaada wenu</p> <p>12. Roho zetu zinazidi kupukutika</p> <p>13. Vijana wetu wanakufa sana</p> <p>14. Vifo vyao havieleweki wala kuelezeaka</p> <p>15. Ngenyile amekatwakatwa na mapanga usiku</p> <p>16. Tupoghile amekunywa sumu</p> <p>17. Vifo vyao namna hii havikuwapo hapo awali</p> <p>18. Tunajiuliza kuna nini huko?</p> <p>19. Tunaomba, muulizane na ninyi huko mtusaidie majanga haya yaishe na yasijirudie tena</p> <p>20. Tunaomba mzidi kuwalinda watoto hawa</p> <p>21. Tunaomba mtuhurumie na katuombea kwa Mungu watoto wetu wakue vizuri, wasome na wasijiingize kwenye mambo ya kidunia</p> <p>22. Tumewaletaa pombe, unga na nyama hiyo</p> <p>23. Mle wote na mzidi kutusaidia tuzidi kuwa na amani na ushirikiano</p>

**Chanzo:** Uwandani (2020)<sup>4</sup>

Data hii ni ushairi wa tambiko la kuondoa mkosi wa vifo. Tambiko hilo limewasilishwa kwa kutumia muundo huru wa kishairi yaani, usiozingatia kanuni na kaida za kiutunzi za kimapokeo, yaani hakuna urari wa vina na mizani. Kwa mfano, mshororo wa kwanza una mizani 6 ilhali mshororo wa pili una mizani 10 na mshororo wa tatu una mizani 15. Utufauti huo wa mizani unajidhihirisha kwenye mishororo yote iliyoukuliwa katika data hiyo. Kwa upande wa vina tunaona mstari wa kwanza na wa

<sup>4</sup> Tafsiri zote ni za mtafiti.

pili una vina vilivyofanana *-di* ilhali mstari wa tatu una kina *-po*, wa nne *-nda* na wa tano *-nyo*. Utufauti wa vina unajitokeza katika data zote zilizonukuliwa katika makala hii. Muundo huu huruhusu uhuru katika idadi ya mishororo kulingana na mtambikaji mwenyewe. Halikadhalika, idadi ya beti haifanani kwani kuna matambiko yenye beti mbili, tatu, nne na kuendelea. Idadi ya beti imefungwa katika ujumbe, na jambo kubwa linalozingatiwa katika ushairi huu ni maudhui yanayowasilishwa. Pia, ukitazama data hii utaona kuwa tambiko hilo lina muundo wa moja kwa moja na maneno yanayotamkwa wakati wa utambikaji yapo katika mtiririko wa kishairi. Muundo huo unajidhihirisha kuanzia kwenye hatua ya kwanza ya utangulizi ambayo ni ubishaji wa hodi na utambulisho, hatua ya pili ambayo ni kiini (upelekaji wa maombi) na hatua ya mwisho ya utoaji sadaka. Mtiririko huu unajitokeza katika data zote zilizowasilishwa katika makala hii.

Halikadhalika, katika data hii mbinu ya kishairi inazidi kujidhihirisha kupitia matumizi ya mtindo wa uzungumzaji ambao umejengwa katika matumizi ya sentensi fupifupi. Kwa mfano, ukitazama sentensi zote katika data hiyo utabaini kuwa ni fupifupi na ambazo mtambikaji huzitamka kwa kupumzika. Mtindo huu wa uzungumzaji hutumika kwa lengo la kuipatia nafasi hadhira kusikiliza na kuelewa kile kinachowasilishwa na mtambikaji. Sentensi hizo zipo katika ubeti mmojammoja ambao ndani yake kumesheheni matumizi ya mbinu mbalimbali za kisanaa kama vile matumizi ya lugha ya picha, takriri, nyimbo, na mafumbo ambayo ndiyo yamebeba ujumbe na maudhui yaliyokusudiwa. Kwa mantiki hii, lugha na mpangilio wa kishairi ndivyo vinavyotawala uwasilishaji wa tambiko. Zaidi ya mbinu hizi za kisanaa, tunaona uwasilishaji wa matini ya tambiko umefungwa katika matumizi za sauti ambapo sauti ya ughani ndiyo inayotumika kuwasilisha maudhui lengwa. Hapa tunazungumzia sauti iliyo katikati ya uimbaji na uzungumzaji. Kimsingi, vipengele hivi vya kifasihi ndivyo vinavyolijenga, kulikamilisha, kulipambanua na kulipa uhai tukio la utambikaji.

## **6.2 Matumizi ya Takriri**

Takriri ni mbinu ya urudiaji wa kukariri. Mara kadhaa, urudiaji huu unaweza kupatikana katika ngazi mbalimbali kama takriri vina, mizani, neno, mstari na kifungu (Wamitila, 2004). Lengo la matumizi ya takriri ni kuonesha msisitizo wa jambo linalozungumziwa, kuvuta umakini wa wasikilizaji na kusaidia kuibua maudhui. Takriri ni kipengele kimojawapo kinachojitokeza sana katika utendaji wa tambiko. Ujitokezaji huo huanzia katika hatua ya ufunguzi wa tambiko ambapo kiongozi wa tambiko hutakiwa kufanya mawasiliano na hadhira lengwa ambayo ni wahenga na miungu. Mawasiliano hayo huanza kwa kubisha hodi mara tatu kisha kurudia tena mara moja na kuwataja wahenga wao. Kitendo cha kubisha hodi mara tatu kwa awamu ya kwanza hulenga kuwapa taarifa wahenga na mizimu kuwa kuna ugeni, hivyo, wanapaswa kuupokea. Aidha, kitendo cha kurudia mara mojamoja na kuwataja wahenga ni kuonesha kuwatambua, kuwapa thamani na kuonesha utayari wa kuanza kuwasiliana nao. Mbinu hii ya matumizi ya takriri inajidhihirisha katika matambiko ya Wapangwa kama inavyoonekana katika Data Na. 2 ambayo ni sehemu ya ufunguzi wa tambiko la kuondoa mikosi ya vifo vya kushtukiza, Data Na. 3 ni sehemu ya ufunguzi

wa tambiko la kushukuru kwa kupata mtoto wa kiume, na Data Na. 4 ni ufunguzi na kiini cha tambiko la kuondoa mkosi wa kutokuolewa kama ifuatavyo:

(2)

<i>Iliteghelo lyaghuhongecha ughupata umwana</i>	<b>Tambiko la shukurani ya kupata mtoto</b>
<ol style="list-style-type: none"> <li>1. <i>Hodi hodi hodi</i></li> <li>2. <i>Hodi! nyevakughu nyevagoyo</i></li> <li>3. <i>Nyevakughu yemwatulongwe</i></li> <li>4. <i>Nyevakughu nyevasughu</i></li> </ol>	<ol style="list-style-type: none"> <li>1. Hodi! Hodi! hodi!</li> <li>2. Hodi! enyi mababu watukufu</li> <li>3. Hodi! Wahenga mliotutangulia</li> <li>4. Mababu wenyе utashi</li> </ol>

**Chanzo:** Uwandani (2020)

(3)

<i>Iliteghelo lyaghuhonge cha ughupata umwana</i>	<b>Tambiko la kushukuru kwa kupata mtoto</b>
<ol style="list-style-type: none"> <li>1. <i>Hodi! Hodi! Hodi!</i></li> <li>2. <i>Hodi! nyevakughu vetu</i></li> <li>3. <i>Nyevavina vamateghelo agha</i></li> <li>4. <i>Nyevakughu nyevatwa</i></li> </ol>	<ol style="list-style-type: none"> <li>1. Hodi! Hodi! Hodi!</li> <li>2. Hodi! Mababu zetu</li> <li>3. Hodi! Wakuu wa mbari hii</li> <li>4. Mababu watukufu</li> </ol>

**Chanzo:** Uwandani (2020)

(4)

<i>Iliteghelo ilya kuhecha imikosi iyaghukosa ughughegha nughughegwa</i>	<b>Tambiko la kuondoa mkosi wa kutooa na kutoolewa</b>
<ol style="list-style-type: none"> <li>1. <b><i>Hodi! Hodi! Hodi!</i></b></li> <li>2. <b><i>Hodi vakughu nyevagoyo...</i></b></li> <li>3. <b><i>Avahinjava vadughile lino na</i></b></li> <li>4. <b><i>Avahinjava valeghaghe ughuholela munyumba</i></b></li> <li>5. <b><i>Avahinjava valeghaghe ughukosa avaghosi avaghuvaghegha</i></b></li> <li>6. <b><i>Avahinjava vaghavangagke inyumba chavo...</i></b></li> </ol>	<ol style="list-style-type: none"> <li>1. Hodi! Hodi! Hodi!</li> <li>2. Hodi! Mababu mliotukuka...</li> <li>3. Mabinti zetu wanakoma sasa na uzao tutakosa</li> <li>4. Mabinti zetu wasizalie nyumbani</li> <li>5. Mabinti zetu wasikose waume wa kuwaoa</li> <li>6. Mabinti zetu wakajenge familia zao zenye heshima...</li> </ol>

**Chanzo:** Uwandani (2020)

Katika madondoo haya tunaona matumizi ya takriri neno “*Hodi! hodi! hodi!*” ambalo limerudiwa mara tatu kisha mara mojamoja. Neno ‘hodi’ halijarudiwa kimakosa bali ni kwa kusudi maalumu kama kuomba ridhaa ya kuanza kufanya mawasiliano, kusisitiza jambo, kuamsha hisia za wasilikizaji na kuleta umakini katika kupokea ujumbe.

Utumizi wa mbinu hii katika matambiko unadhihirisha ufasihi uliopo katika matambiko hayo.

### **6.3 Matumizi ya Lugha ya Picha**

Lugha ya picha huhusisha matumizi ya jazanda, taashira, taswira na ishara mbalimbali ambazo hutumika kuashiria kitu kingine. Hii ni lugha inayochora picha ya watu, vitu au mahali kwa kutumia ishara na alama mbalimbali. Katika matambiko, kuna matumizi ya lugha ya picha kama vile taashira ambazo zimetumika kuashiria kitu fulani kilichokusudiwa. Kwa mfano, katika tambiko la shukrani ya kupata mtoto wa kiume, tunaona kiongozi wa tambiko anafanya mawasiliano na wahenga. Katika mawasiliano hayo anatumia neno “*imbeyu*” yaani, “mbegu” anaposema “*Imbeyu yeyakangye nughumela vunofi*” akiwa na maana ya kwamba wameenda kuwashukuru kwa zawadi waliyoipata na zawadi hiyo imetokana na ‘mbegu walizozipanda ambazo zilikomaa na kumea vizuri’. Hapa neno ‘mbegu’ limetumika kuashiria mchakato mzima wa uzalishaji yaani, wameenda kushukuru kwa kupata zawadi ya mtoto na wanaamini mtoto huyo ametokana na urijali, nguvu, uimara na uwezo wa kiuzao waliokuwa nao vizazi viliviyotangulia. Haya yanajitokeza katika Data Na. 5 inayohusu tambiko la kushukuru kwa kupata mtoto wa kiume kama ifuatavyo:

(5)

<b>Iliteghelo lyaghuhonge cha ughupata umwana</b>	<b>Tambiko la shukrani ya kupata mtoto</b>
<ol style="list-style-type: none"> <li>1. <i>Twichile ghuhongecha ughutupela isawadi iyi</i></li> <li>2. <i>Iyi imbeyu yemwayalile</i></li> <li>3. <i>Imbeyu yeyakangye nughumela vunofi</i></li> <li>4. <i>Agha ghematunda ghaghe</i></li> <li>5. <i>Twichile ghuvonola ghwenyo umwana venyo umudimi uyu...</i></li> </ol>	<ol style="list-style-type: none"> <li>1. Tumekuja kuwashukuru kwa zawadi hii</li> <li>2. Zawadi iliyotokana na mbegu mlizozipanda</li> <li>3. Mbegu zilizokomaa na kumea vizuri</li> <li>4. Zawadi hii ni matunda yake</li> <li>5. Tunamleta na kumkabidhi kwenu mtoto wetu wa kiume...</li> </ol>

**Chanzo:** Uwandani (2020)

Ukitazama dondo liliopo katika Data Na. 5, utaona kuna matumizi ya taashira, yaani mbegu imetumika kwa malengo maalumu huku ikiashiria mchakato mzima wa uzalishaji hadi kupatikana kwa kiumbe.

Vilevile, katika Data Na. 6 hapo chini tunaona matumizi ya neno “maua” na “majembe”. Hizi ni taswira ambazo zimetumika katika tambiko zikiwa na maana mbalimbali. Kwa mfano, “maua yalichanua” imetumika kuashiria mabinti ambao bado hawajaolewa huku “majembe” ikitumika kuashiria mchakato wa uoaji. Taashira hizi zinajitokeza katika Data Na. 6 kama ifuatavyo:

(6)

<b>Iliteghelo ilya kuhecha imikosi iyaghukosa ughughegha nughughegwa.</b>	<b>Tambiko la kuondoa mkosi wa kutokuolewa</b>
<ol style="list-style-type: none"> <li>1. ...<i>Ululuva lughahomwe lino ve lwighuma</i></li> <li>2. <i>Tulindili gheamaghimilo lino situghaghavona</i></li> <li>3. <i>Ulukelo ghuno sighthweluli</i></li> <li>4. <i>Twinyiligha mututange</i></li> <li>5. <i>Tupiluse ulukelo lywetu ulwaghatali</i></li> <li>6. <i>Mutunyilighilaghe ghwanguluvi mukosi ughu ghusile</i></li> </ol>	<ol style="list-style-type: none"> <li>1. ...Maua yalichanua na sasa yananyauka</li> <li>2. Tumesubiri majembe lakini hatujayaona</li> <li>3. Heshima haipo tena</li> <li>4. Tunaomba msaada wenu</li> <li>5. Heshima na fahari yetu irudi kama awali</li> <li>6. Mtuombee kwa Mungu, mkosi huu uishe</li> </ol>

**Chanzo:** Uwandani (2020)

Katika Data Na. 6 hapo juu, tunaona matumizi ya taswira yanajitokeza hasa fanani mkuu anaposema, “*Ululuva lughahomwe lino ve lwighuma*” akiwa na maana ya kwamba “maua yalikuwa yamechanua na sasa yananyauka” kinachomaanishwa hapa ni kwamba ‘watoto wao wa kike walifika umri wa kuolewa na sasa wamepita umri huo bila kuolewa’. Pia, kuna matumizi ya taswira yanayojidhihirisha kuitia neno “*amaghimilo*” wanaposema “*Tulindilighe amaghimilo lino situghaghavona*” yaani, “tumesubiri majembe lakini hatujayaona” maana yake wamesubiri ‘waoaji wa kuja kujitambulisha, kutoa posa na kuo mabinti zao lakini jambo hilo halikufanikiwa’. Mchakato huo wa uoaji umefungamanishwa na utamaduni asilia wa Kipangwa. Utamaduni huo hujidhihirisha pale kijana anapotaka kwenda kuposa sehemu hupaswa kutoa taarifa kwa familia yake ili kuanza taratibu husika. Miongoni mwa taratibu muhimu za mwanzo ni kuandaa jembe na kwenda nalo katika familia ya kike ambayo mtoto wao anataka kuo. Jembe hilo hufikishwa nyumbani hapo asubuhi na mapema kabla wenyeji hawajaamka na kuwekwa uwanjani. Hivyo, wenyeji watakapoamka na kufungua mlango watalikuta jembe hilo. Hii huwa ni ishara ya kuwa kuna kijana ambaye amempenda binti wa familia hiyo na anakusudia kumuoa. Kinachobainika hapa ni kwamba matumizi ya lugha ni kipengele muhimu kinachotumika katika uwasilishaji wa tambiko na kudhihirisha ufasihhi wake.

#### **6.4 Matumizi ya Nyimbo**

Nyimbo ni utungo wa kisanaa unaowasilishwa kimuziki kwa kutumia sauti iliyo katika mpangilio fulani wa mahadhi, melodia, na wenyе mapigo ya kiurari (Mulokozi, 2017). Nyimbo ni utanzu muhimu katika matambiko na kila tambiko huwa na nyimbo zinazofungamana na utendaji wake. Nyimbo hizo huwa na matini au maneno yanayoimbwa ambayo hubeba na kufungamana na maudhui ya tambiko husika, huwa na muziki wa sauti ya muimbaji au waimbaji ambaо hujumuisha mapigo na mahadhi yake, matumizi ya ala za muziki kama vile ngoma na zeze, hadhira inayoimbiwa na

muktadha unaofungamana na wimbo huo ambao sasa ndiyo tambiko lenyewe. Nyimbo za tambiko husaidia kuelewa kusudi la tambiko lililofanyika ikiwa na maana kwamba nyimbo lazima zibebe maudhui ya tambiko husika.

Katika utendaji wa matambiko ya Wapangwa, nyimbo haziimbwi wakati wa tambiko husika bali huanza kuimbwa mara tu kiongozi wa tambiko anapomaliza utambikaji. Uimbaji huo huendelea mpaka watakapofika nyumbani na kupokelewa na wanaukoo pamoja na watu mbalimbali walioalikwa kwa ajili ya tambiko hilo. Nyimbo hizo huimbwa mpaka siku ya tatu ambayo kwa kawaida ndiyo siku ya mwisho ya kumalizia tambiko. Umalizaji wa tambiko hudhihirika hasa baada ya wahusika wa tambiko kuongozana na kiongozi wao mpaka kwenye eneo husika walilofanyia tambiko ili kuangalia kama mababu wamepokea vitu walivyopelekewa ambavyo ni pombe, nyama na unga. Baada ya kuona vitu hivyo havipo, watambikaji huamini kwamba wahenga wamepokea na wapo tayari kuyajibu maombi yao na ndipo huanza kuimba nyimbo zinazofungamana na tambiko husika. Lengo la uimbaji huo ni kuashiria furaha kwa kupata kibali na huwa ndiyo mwisho wa tambiko husika. Kwa mantiki hiyo, nyimbo ni kipengele muhimu katika ufanikishwaji na ukamilishaji wa tambiko husika. Haya yanajidhihirisa katika Data Na. 7 na Data Na. 8 zinazohusu nyimbo za tambiko zilizoimbwa ili kukamilisha tambiko la shukrani ya kupata mtoto kama ifuatavyo:

(7)

<i>Ulwimbo lwa liteghelo lyaghuholwa</i>	<b>Wimbo wa tambiko la uzazi</b>
1. <i>Ulughanga lwetu lupatile lufunyo</i>	1. Ardhi yetu imepata neema
2. <i>Ulughanga lwetu lupatile ibalagha</i>	2. Ardhi yetu imepata baraka
3. <i>Ulughanga lwivonesa ughuva imbeyu iyi yatunjijwe vunofi nughukangala</i>	3. Ardhi yetu yaonesha mbegu ilitunzwa na kukomaa
4. <i>Imbeyu iyi yendelelaghe ughukula</i>	4. Mbegu hii itazidi kuimarika
5. <i>Imbeyu iyi yendelelaghe ughwologha</i>	5. Mbegu hii itazidi kusambaa
6. <i>Oyelele Ooh Yelelele!! X2</i>	6. Oyelele! Ooh! Yelelele!! x2
7. <i>Mwiche uve muyetu</i>	7. Je uwe mmoja wetu
8. <i>Wiche tuvepamwi</i>	8. Uje uwe sehemu yetu
9. <i>Wiche tughulele na ghwilela</i>	9. Uje utunzwe na kujitunza
10. <i>Uve lufunyo</i>	10. Uzidi kuwa neema
11. <i>Wongeleche ishog'hela ghikulaghe</i>	11. Uzaliane na kuongeza vizazi
12. <i>Unochaghe ghwenivala ghuno</i>	12. Uupambe ulimwengu
13. <i>Unochaghe ughwologha</i>	13. Uupambe kwa uzao
14. <i>Ghivechagke shong'ela shamana</i>	14. Uzao wenye manufaa

(8)

<i>Ulwimbo lwa ghukamilisa iliteghelo lwighwimbwa ighighono ishavuvili</i>	<b>Wimbo wa kukamilisha tambiko la kushukuru kwa ajili mtoto</b>
<ol style="list-style-type: none"> <li>1. <i>Avakughuyo vaghwanushe</i></li> <li>2. <i>Ilelo iyi vanyalukelo</i></li> <li>3. <i>Ughwicha ghwagho vikelye</i></li> <li>4. <i>Ughwicha ghwagho ghughatulimba tuve lumwi</i></li> <li>5. <i>Ukulagke uvechagke mnofi gwetu nughwavo</i></li> <li>6. <i>Ghusudi vendelelaghe ughutunyilighila ghwa Nguluvi atupelaghe amanofi</i></li> <li>7. <i>Wichagke muinyi iyi</i></li> <li>8. <i>Ukulagke wongelechaghe ishong'ela ighi x3</i></li> </ol>	<ol style="list-style-type: none"> <li>1. Nao mababu wamekupokea</li> <li>2. Leo hii wanasherehekeea</li> <li>3. Ujio wako umewafurahisha</li> <li>4. Ujio wako umezidi kutuunganisha</li> <li>5. Ukue uzidi kuwakumbuka na kuwapendeza wao na sisi</li> <li>6. Ili wazidi kutuombea kwa Mungu na kutujalia yaliyo mema</li> <li>7. Karibu katika ulimwengu huu</li> <li>8. Ukue vyema, uje uongeze kizazi hiki x3</li> </ol>

**Chanzo:** Uwandani (2020)

Dondoo katika Data Na. 8 ni wimbo ambao huimbwa siku ya tatu baada ya tambiko. Wimbo huu huimbwa mara tatu tu na hawapaswi kuzidisha kuuimba. Dhana ya kuimba wimbo huu mara tatu ni kuonesha ukamilifu wa tukio husika la utambikaji. Kwa mantiki hiyo, tukio la utambikaji linakamilishwa na nyimbo ambazo huimbwa na watambikaji ili kukamilisha tukio husika. Matumizi ya nyimbo hizo hudhihirisha ufasihi wa tukio la utambikaji.

### 6.5 Matumizi ya Tabano

Tabano ni kipera kimojawapo cha fasihi simulizi kinachohusisha mazungumzo, maongezi au maelezo ya mdomo yenyenye usanii na ambayo hutumia lugha ya kawaida katika kuelezea jambo lolote lile. Tabano ni manuizo asemayo mganga na wapambe wake wakati wa kumtibu mwele (mgonjwa) kijadi. Shughuli nzima ya aina hiyo ni mviga ambao huhusisha watu, mizimu na miungu katika kutafuta ufumbuzi wa tatizo lililojitokeza (Mulokozi, 2017). Lengo la kufanya hivyo ni kutaka kugundua chanzo cha tatizo ikiwa ni la kawaida la mwili, hasira ya mizimu au wahenga ama kulogwa na watu wabaya. Tabano ni kipera kimojawapo kinachodhahirisha ufasihi uliopo katika matambiko. Ufasihi huo unajipambanua katika tambiko kwani tukio la utambikaji huhusisha mazungumzo na maelezo ya mdomo yenyenye usanii, lugha teule, na ni mviga unaohusisha watu, mizimu, wahenga na miungu katika kutatua matatizo mbalimbali kama vile magonjwa, na mikosi inayowakabili. Ufasihi unaojidhahirisha katika tabano unajitokeza pia katika matambiko kupitia manuizo yanayotolewa na kiongozi wa ukoo akiwakilisha ukoo mzima hususani anapozungumza na wahenga, mizimu na mababu juu ya matatizo mbalimbali yanayowakabili. Kwanza, katika matambiko kuna utajaji wa majina ya wahenga, yaani mababu waliokwishakufa zamani kisha kuwaauliza kama

wao ndio wanaohusika na matatizo yanayojitokeza katika jamii au la. Mwisho, ni kuomba radhi na msaada ili kuweza kutatuliwa matatizo hayo. Haya yanajidhihirisha katika Data Na. 9 kama ifuatavyo:

(9)

<b>Illiteghelo lyaghuhuhecha imikosi</b>	<b>Tambiko la kuondoa mikosi (vifo)</b>
<ol style="list-style-type: none"> <li>1. <i>Hodi hodi hodi</i></li> <li>2. <i>Hodi nyevakughu nyevagoyo</i></li> <li>3. <i>Hodi! Masasi, Lutangilo na Njelekela</i></li> <li>4. <i>Nyevakughu yemwatulongwe</i></li> <li>5. <i>Yemwimanya amavivi na manofi</i></li> <li>6. <i>Twichile twevana venyo tweva Habilo, Mbwatalilo na Lugome</i></li> <li>7. <i>Twinyiligha mutwanughile nughutupulighicha</i></li> <li>8. <i>Twevayinjo ghuno tunyamola makomi isichisila</i></li> </ol>	<ol style="list-style-type: none"> <li>1. Hodi hodi hodi!</li> <li>2. Hodî enyi mababu watukufu</li> <li>3. Hodî! Masasi, Lutangilo na Njelekela</li> <li>4. Enyi mababu mliotangulia</li> <li>5. Mnaojua mema na mabaya</li> <li>6. Tumekuja sisi watoto wenu wakina Habilo, Mbwatalilo na Lugome,</li> <li>7. Tunaomba mtupokee na kutusikiliza</li> <li>8. Huku tuna matatizo makubwa yasiyoisha</li> </ol>

**Chanzo:** Uwandani 2020

Dondoo hili ni tambiko la kuondoa mkosi wa vifo. Tunapochunguza tambiko hilo, tunabaini kuwa kuna matumizi ya majina ya wahenga anaposema, “*Hodi! Masasi, Lutangilo, na Njelekela*” anaonesha imani yao juu ya wahenga ya kwamba wapo, wanaona, wanasikia na wanajibu maombi wanayoombwa ijapokuwa wahenga hao hawajidhihirishi katika hali ya kawaida. Katika kushadidia hilo, Mulokozi (2017) anaeleza juu ya ufasihî uliopo katika tabano. Anasema kuwa njia mojawapo inayohusiana kidogo na fasihi ni ile ya kumtaka (mwele) mganjwa awataje kwa majina wahenga wake waliokwishafariki. Baada ya hapo mganga hutumia tunguri zake kunuiza tabano huku akitaja jina mojamoja na kumwuliza mhusika (mhenga) kama anahusika na tatizo hili, na kwa nini. Je, mwanawe kamkosea jambo na anahitaji lirekebishwe? Je, amenyimwa tambiko lake? Katika hatua hii, nyimbo maalumu huimbwa na mganga huku akiitikiwa na wapambe wake au watu waliopo; wakati mwingine hata ala za muziki kama zeze, nanga au ngoma hutumika. Huu ni mfano mzuri wa namna fasihi simulizi inavyotumika katika maisha halisi na kufanikisha kutekeleza lengo fulani la kimaisha (Mulokozi, 2017: 89-90). Kutokana na maelezo hayo, ni wazi kuwa tambiko ni kipera kimojawapo cha fasihi kwa sababu kimebeba sifa za fasihi simulizi ambazo hudhihirika kuititia utendaji na uwasilishaji wake.

## 6.6 Matumizi ya Balagha

Balagha ni utiaji chuku au chumvi. Hapa huweza kuongeza au kupunguza maneno katika ujumbe fulani kwa lengo la kusositiza, kusifia kitu fulani au kuchekesha. Mbinu hii hutumika sana katika utendaji wa matambiko. Mtambikaji anapotambika huhusisha

utiaji wa chuku kuhusu uwezo wa viumbe, tabia pamoja na sifa zao kwa madhumuni ya kusisitiza. Kwa mfano, mtambikaji anaposema, “wahenga mliotukuka, mababu mnaoishi milele, mababu watukufu, mnaoishi milele, mnaosikia tusiyoyasikia na mnaoona tusiyoyaona...”. Ukifuatilia mazungumzo haya, utabaini kuwa wahenga hawa wanapewa sifa nyingi za kiutendaji ambazo si za kawaida na ni vigumu kuthibitisha ufanyaji kazi na udhihirikaji wake. Tazama Data Na. 10 inayooonesha namna balagha inavyojidhihirisha katika dondoo la tambiko la kuondoa mkosi wa kutokuolewa kama ifuatavyo:

(10)

<i>Iliteghelo lyakuhola umwana</i>	<b>Tambiko la uzazi</b>
1. Nyevakughu nyevatwa	1. Mababu watukufu
2. Yemwitama isighu jchonda	2. Mnaoishi milele
3. Yemwilola ghesitughaghavona	3. Mnaoona tusiyoyaona na
4. Yemwipuligha ghesitwipuligha	4. Mnaosikia tusiyoyasikia

**Chanzo:** Uwandani (2020)

Katika dondoo hili la tambiko la kuondoa mkosi wa kutokuolewa, tunaona namna wahenga wanavyotazamwa na wanajamii husika hasa kwa kupewa uwezo mkubwa wa kutenda, kupambwa kwa maneno mazuri yanayoonesha uwezo na nguvu zao za kiutendaji. Fikra hizi zimejengwa katika imani na mitazamo ambayo imefungwa katika falsafa ya Kiafrika ya kwamba kuna maisha baada ya kifo na wahenga huishi maisha ya milele huku wakiwa na jukumu la kuwasaidia walio hai kufanikisha maisha yao (Mbiti, 1991). Mbali na fikra hizi za kifalsafa, tunaona mtambikaji akisema, “mababu watukufu”, “mnaoona tusiyoyaona”, “mnaosikia tusiyosikia” akiwa na maana kuwa wahenga wanatazamwa kuwa ni viumbe safi, wasiokuwa na dhambi yoyote na wenye uwezo fulani wa kipekee wa kuona, kusikia na kutenda matendo mbalimbali ambayo binadamu wa kawaida hawezikuyatenda. Huu ni uongezaji chumvi wa wazi ambao unaonesha namna watambikaji wanatoa sifa nyingi kwa wahenga kwa kuwatukuza, kuonesha nguvu na nafasi yao katika maisha ya waliohai. Hivyo, balagha ni kipengele kimojawapo muhimu kinachodhihirisha ufasihi wa matambiko. Kupitia balagha tunaona kuwa utambikaji ni sanaa ambayo huhitaji ubunifu na uteuzi wa maneno ambayo huweza kuvuta hisia, umakini na shauku ya wasikilizaji.

## 6.7 Utendaji wa Kifasihi Simulizi

Hapa tunajiegemeza katika muktadha wa kiutendaji wa matambiko kwa kuzingatia misingi ya kifasihi simulizi. Ikumbukwe kuwa fasihi simulizi huwa na muktadha wa utongoaji wake na ndiyo unaoitofautisha na fasihi andishi. Utotfauti huo unatokana na sababu kwamba fasihi simulizi ni lazima itendwe ndipo ikamilike. Mulokozi (2017) anapoeleza juu ya utendaji wa fasihi simulizi, anasema kwamba ikitokea fasihi ikatendwa kwa njia tofauti, wakati tofauti, kwa hadhira tofauti, na fanani tofauti huwa ni utungo tofauti. Kimsingi, utungo simulizi ni sanaa inayopita, isiyo na maisha au uendelevu nje ya utendwaji wake. Kwa mantiki hiyo, kazi yoyote ya fasihi simulizi sharti itendwe kwanza ndipo ikamilike. Utendaji simulizi ni dhana inayotumika

kuelezea mtindo wa kuwasilisha tungo sambamba na kuwapo kwa matendo kama uigizaji, sauti na matumizi ya ishara (Wamitila, 2003). Utendaji ni dhana inayohusisha uwasilishaji wa jambo fulani mbele ya hadhira na hulusisha kuwapo kwa mwingiliano baina ya mambo muhimu ambayo ni fanani, hadhira, fani inayotendwa, muktadha wa utendaji, maudhui yanayoelezwa, tukio, kusudio la utendaji na wakati. Kuwapo kwa utendaji ni mojawapo ya mambo muhimu ambayo huutambulisha na kuupambanua utanzu wa fasihi simulizi. Kwa sababu hiyo, matini ya tambiko pekee haiwezi kuwa fasihi simulizi pasipo kuhusisha utendaji ambao hujikita katika uchambuzi wa vipengele vinavyotamkwa ambavyo ni pamoja na mtindo na maudhui, jazanda au pengine upokezani (wa fasihi hiyo).

Ufasihi wa tambiko unaanza kujitokeza kuanzia kwenye tukio lenyewe la utambikaji. Tukio la utambikaji ni la kifasihi simulizi kwa sababu limefungwa katika sifa kuu za kiutendaji za fasihi simulizi. Sifa hizo ndizo zinazolipambanua na kulipa maana tambiko husika. Tutazame udhihirikaji wa sifa hizo katika tambiko: kwanza, kuwapo kwa fani inayotendwa; hapa tunazungumzia ile sanaa yenyewe inayotendwa ambayo kimsingi ndilo tambiko lenyewe. Tukio zima la utambikaji ni la kisanaa na ndiyo fani mahususi ambayo inatendwa na fanani mkuu mbele ya hadhira husika. Tukio la utambikaji hulusisha sanaa ya lugha ambayo imefungwa katika mazungumzo ya mdomo ya fanani mkuu, utumizi wa ishara na vitendo (lugha ya kiishara) pamoja na nyimbo. Pili, kuwapo kwa maudhui yanayoelezwa; hii ni taarifa, dhamira, ujumbe ambao fanani anauwasilisha kwa hadhira. Hapa ni wazi kuwa tambiko hufanyika kutokana na dhununi maalumu ambalo wanaukoo wakiongozwa na fanani mkuu huhitaji kuliwasilisha kwa hadhira ambao ni wahenga. Hivyo, utendaji wa tambiko hutegemea maudhui lengwa ambayo yanapaswa kufikishwa kwa miungu yao. Mfano mzuri wa hili unajitokeza katika Data Na. 4 ambalo ni dondoo la tambiko la kuondoa mkosi wa kutokuolewa. Tunaona maudhui makuu yanayobainika katika data hiyo ni umuhimu wa ndoa na kwamba mabinti wakiingia kwenye ndoa huwa ni heshima na furaha kwa wazazi na mabinti wenyewe.

Tatu, mandhari au mahali; huu ni uwanja wa kutenda. Tambiko hufanyika katika mazingira maalumu hususani kwenye milima, misitu, miti mikubwa na kwenye makaburi. Sehemu hizo ni zile zilizokuwa zikitumiwa na mababu toka zamani na hurithishwa toka kizazi hadi kizazi. Maeneo hayo ni lazima yawe yamebeba historia ya vizazi viliviyotangulia na hata kuwa na majina ya mababu wa zamani. Hivyo, tambiko ni sanaa ambayo hufanyika kwa kuzingatia eneo mahususi la kiutendaji. Nne, wakati wa kiutendaji; hapa tunazungumzia muda maalumu kihistoria au majira maalumu ya kiutendaji. Matambiko ya Wapangwa hufanyika katika kipindi maalumu hususani kuanzia mwezi wa nane mpaka wa kumi na moja, kipindi cha kiangazi ambapo wanajamii huwa wamemaliza shughuli zao za shamba. Pia, kuna matambiko ambayo hufanyika kutegemea na uhitaji maalumu, kwa mfano, tambiko la ugonjwa, vifo vyaa ghafla na kumhamisha marehemu. Hivyo, kuwapo kwa muda maalumu wa kiutendaji kunabainisha kuwa tambiko limefungwa katika sifa pambanuzi za kifasihi similizi.

Tano, kuwapo kwa tukio husika ambalo hulusisha shughuli au kadhia ya kijamii ambayo ndiyo muktadha wa utendaji huo wa sanaa. Shughuli hiyo ya kijamii ni kuwapo kwa tukio lenyewe la kiibada, yaani tambiko ambalo hufanyika na ndilo

linalokamilisha dhana nzima ya utendaji. Sita ni kuwapo kwa wahusika; tambiko huhusisha wahusika ambao ndio watendaji wakuu wa tambiko. Wahusika hawa ndio nyenzo na nguzo kuu katika ufanikishwaji wa kazi yoyote ile ya fasihi na hubeba maudhui yaliyokusudiwa ambayo huwakilishwa kuitia uhusika wao. Wahusika wa tambiko wamegawanyika katika sehemu mbili ambapo kuna upande wa fanani na hadhira (taz. Mhando, 1976). Tunapozungumzia wahusika wanaopatikana katika tambiko, ni muhimu kujua kwamba upande wa fanani huwa ndiyo wasemaji wakuu, yaani hueleza malengo na maombi yao kwa miungu. Fanani (viongozi wa tambiko, wakuu wa koo au mila, au mtani ambao huteuliwa kuongoza tambiko husika, wanaukoo au wanafamilia) ni watu walio hai na hujidhihirisha kiutendaji katika hali ya kimwili. Upande wa pili, huhusisha hadhira, yaani wasikilizaji na wapokeaji wa maombi. Hadhira huhusisha miungu, wahenga, mizimu na mahoka ambao ni mababu wa kale, waliokufa zamani. Hii ni hadhira dhahania ambayo hajidhihirishi katika hali ya kimwili, hawaonekani katika hali ya kawaida na hata utendaji wake haudhihiriki wazi wakati wa utendaji wa tambiko. Hata hivyo, licha ya kutoonekana, hadhira hii huaminika kwamba ipo, inaona, inasikia na inajibu yale yanayoombwa na wanajamii, yaani ni hadhira iliyopo akilini mwa fanani.

Kwa kuwa si kila mtendaji huashiria ufasihii katika tambiko, hapa tunamzungumzia fanani mkuu ambaye ndiye mtambikaji. Fanani mkuu amejengwa katika misingi ya kifasihi simulizi ambayo hujidhihirisha kutokana na namna anavyowasilisha tukio husika la utambikaji. Kwa mfano, kiuwasilishaji fanani mkuu anafungwa katika matumizi ya lugha ya kisanaa (mazungumzo ya mdomo yenye usanii na ubunifu ndani yake), uteuzi wa lugha, maneno na miundo ambayo inawakilisha mtindo huru wa kishairi uliojazwa lugha ya mafumbo, takrir na lugha ya picha, mtindo wa uzungumzaji hapa ndipo matumizi ya sauti hujidhihirisha kwani sauti inayotumika ni ile ya ughani, yaani iliyo kati ya uimbaji na uzungumzaji. Utumizi wa ishara na vitendo, matumizi ya sauti na mahadhi ya utongoaji katika uwasilishaji wake na uvaaji wa mavazi maalumu, yaani maleba. Uwapo wa wahusika hao unajidhihirisha katika Data Na. 11 inayohusu tambiko la kuondoa mikosi ya vifo kama ifuatavyo:


(11)

<i>Iliteghelo lyaghuhecha imikosi</i>	<b>Tambiko la kuondoa mikosi (vifo)</b>
<ol style="list-style-type: none"> <li>1. <i>Hodi! Hodi! Hodi!</i></li> <li>2. <i>Yunye vakughu nyevaghoyo</i></li> <li>3. <i>Nyevavina yemwavangile ishongela ighi</i></li> <li>4. <i>Twichile twevana venyo</i></li> <li>5. <i>Twinyiligha mutwanughile nughutupulighicha</i></li> <li>6. <i>Unene nde Joni mwana va Lupyana</i></li> <li>7. <i>Unene lino ndivele yemuvina valiteghelo lyetu...</i></li> </ol>	<ol style="list-style-type: none"> <li>1. <i>Hodi! Hodi! Hodi!</i></li> <li>2. <i>Enyi mababu! Mababu mliotukuka</i></li> <li>3. <i>Wakuu na waanzilishi wetu</i></li> <li>4. <i>Tumekuja wanenu</i></li> <li>5. <i>Tunaomba mtupokee na kutusikiliza</i></li> <li>6. <i>Mimi ni Joni mtoto wa Lupyana</i></li> <li>7. <i>Ndiye kiongozi wa mbari yetu kwa sasa...</i></li> </ol>

**Chanzo:** Uwandani (2020)

Katika dondo hili tunaona kuwapo kwa fanani kunajidhihirisha kupitia utamkwaji wa maneno haya: “*Twichile twevana venyo, Unene nde Joni mwana va Lupyana, Tulipamwinga na vayangu ava Lukelo nu Lukengelo,*” yaani “Tumekuja wanenu, mimi ni Joni mtoto wa Lupyana, nimeongozana na wenzangu Lukelo na Lukengelo.” Ukifuatilia, utagundua kuwa kiongozi wa ukoo ndiye fanani mkuu ambaye huzungumza na wahenga na ndiye kiwakilishi cha wanaukoo wengine. Vilevile, anaposema “tumekuja sisi watoto wenu, tunaomba mtusikilize” tunaona kuna matumizi ya wingi kuonesha kuwa suala la tambiko si la mtu mmojammoja bali ni tukio la kijamiii linalohusisha ukoo ama familia ambao kuwapo kwao ni muhimu katika ukamilishaji wa ada hiyo. Kwa upande wa hadhira, tunaona wanajidhihirisha kupitia maneno kama “enyi mababu”, “mababu mliotukuka”. Mazungumzo haya yanaonesha kuwapo kwa mawasiliano maalumu baina ya pande mbili, yaani fanani na hadhira maalumu ambayo hufikishiwa maombi hayo.

Kinachobainika hapa ni kwamba utendaji ndio uti wa mgongo na kiini cha dhana nzima ya tambiko. Utendaji wa tambiko umefungwa katika mwingiliano wa vipengele muhimu vya kifasihi simulizi vinavyodhihirisha muktadha wa utendaji ambaeo ndio unaoamua fani ya tambiko ichukue umbo lipi la fasihi simulizi. Aidha, makala hii imebaini kuwa mazingira ya kiutendaji, sambamba na namna utanzu husika unavyowasilishwa, ndivyo vinavyoupambanua huku vikiathiri uzito na maana ya wasilisho, na ndivyo hulipa uhai tukio la kifasihi simulizi na si matini ya tambiko pekee. Mathalani, mjadala kuhusu ufasihi wa matambiko umetusaidia kufahamu mambo kadhaa. Kwanza, tambiko ni kipera cha fasihi ambacho kinajipambanua kwa kuwa na sifa zote za fasihi simulizi. Pili, tambiko ni dhana pana ambayo huweza kufasiliwa na kutumika kwa namna mbalimbali kulingana na kaida pamoja na matakwa na uga uliokusudiwa; ikiwa na maana kwamba tambiko huweza kutumiwa na wanafasihi, wanahistoria, wanaanthropolojia, wanamithiolojia, wanatheolojia na hata wanafalsafa na kila mmoja akafanikisha kusudi lake kulingana na kaida, yaani taratibu na sheria za uga anaofungamana nao. Mathalani, ili kurahisisha uelewa wa wasomaji juu ya mjadala huu, makala hii imetoa ufanuzi wa mitazamo hiyo miwili kuhusu dhana ya tambiko, ufasihi wake na inavyoweza kujipambanua katika taaluma mbalimbali kama Kielelezo Na. 2 kifuatacho kinavyoonesha:



**Kielelezo Na. 2: Mwingiliano wa tambiko na taaluma nyinge**  
**Chanzo:** Mtafiti (2020)

### 7.0 Hitimisho

Kupitia mjadala huu kuhusu ufasihi wa matambiko, makala hii imebaini yafuatayo: mosi, matambiko hutumia lugha teule ambayo huendana na muktadha wa kiutendaji pamoja na jambo linalowasilishwa. Pili, hutumia mbinu za kielimu-mitindo kama vile takriri, balagha, lugha ya picha, ishara na taswira mbalimbali ambavyo hutumika kwa shabaha maalumu. Vilevile, kuna matumizi ya mtindo wa kishairi katika kufikisha ujumbe. Mtindo huu huzingatia sifa za ushairi huru, uimbikaji, sentensi fupifupi ambazo hukidhi mawasiliano baina ya fanani na hadhira kwani huwa ni mtindo wa mazungumzo ambaa huruhusu upande mmoja kusikiliza. Aidha, kuna matumizi ya nyimbo na tabano. Mwisho ni udhihirikaji wa sifa kuu ya fasihi simulizi ambayo ni utendaji wa kifasihi simulizi. Utendaji huu hujidhihirisha kupitia kuwapo kwa mwangiliano wa vipengele vikuu vinavyoikamilisha na kuipambanua fasihi simulizi, kwa mfano, fani inayotendwa, tukio, muktadha, maudhui na kuwapo kwa fanani na hadhira. Vipengele hivi vyote vinajitokeza katika utendaji wa tambiko na ndivyo hulipa maana na kulikamilisha tukio zima la utambikaji. Kwa mantiki hiyo, ni wazi kuwa matambiko yanakidhi sifa za kuwa kiperia kimojawapo cha fasihi simulizi.

### Marejeleo

- Barndon, R. (2004). *Technology and Morality: Rituals in Iron Working among the Fipa and Pangwa Peoples in Southwestern Tanzania*. Bergen: University of Bergen.
- Bauman, R. (1975). *Verbal Art as Performance*. New Jersey: Blackwell Publishing.
- Dundas, C. (1968). *Kilimanjaro and Its People*. London: New Impression.
- Hassan, H.H. (2013). *Taswira Zinazojitokeza katika Nyimbo za Mwaka-Kogwa. Tasinifu ya Umahiri (Haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam*.
- Hornby, R. (1998). *Oxford Advanced Learner's Dictionary of Current English*. Nairobi: Oxford University Press.

- Mbiti, J. (1991). *Introduction to African Religion*. Nairobi: East African Educational Publishers Ltd.
- Mbonde, J.P. (1973). *Wamakonde*. Masasi: Ndanda Mission Press.
- Mhando, P.O. na Balisidya, N. (1976). *Fasihi na Sanaa za Maonyesho*. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.
- Mohamed, M. (2009). “Mwaka Kogwa na Changamoto zake” katika *Kiswahili*, Juz. 72:108-122.
- Mulokozi, M.M. (2002). *The African Epic Controversy: Historic, Philosophical and Aesthetic Perspectives on Epic Poetry and Performance*. Dar es Salaam: Mkuki na Nyota Publishers.
- Mulokozi, M.M. (2017). *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili*. Dar es Salaam: KAUTTU.
- Mwasaka, S. (2012) *Dhima ya Tambiko katika Jamii ya Wasafwa: Tambiko la Kuaga na Kukaribisha Mwaka*. Tasinifu ya Shahada ya Umahiri (Haijachapishwa) Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Mwakasaka, C.S. (1977). *The Oral Literature of the Banyakyusa*. Dar es Salaam, Dar es Salaam: (Haijachapishwa).
- Ngure, A. (2003). *Fasihi Simulizi kwa Shule za Sekondari*. Nairobi: Phonex Publishers Ltd.
- Samwel, M. na wenzake (2013). *Ushairi wa Kiswahili*. Dar es Salaam: MEVELI Book Publishers.
- Samwel, M. (2013b). *Tamthiliya ya Kiswahili: Kutoka Miviga ya Kidini Hadi Filamu*. Dar es Salaam: MEVELI Book Publishers.
- Samwel, M. (2015). *Umahiri katika Fasihi ya Kiswahili*. Dar es Salaam: MEVELI Book Publishers.
- Schechner, R. (1985). *Between Theatre and Anthropology*. Philadelphia: University of Pennsylvania Press.
- Schechner, R. (2013). (3rd ed). *Performance Studies: An Introduction*. New York: Routledge.
- Swantz, M. (1970). *Rituals and Symbol in Traditional Zaramo Society*. Uppsala: Almqvist and Wiksell.
- TUKI, (2004). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (Toleo la pili). Nairobi: Oxford University Press.
- Turner, V. (1982). *From Ritual to Theatre: The Human Seriousness of the Play*. New York: Perfoming Arts Journal.
- Wallace, B. (1894). The Art of Interpretation. Perfomance of and Beyond Literature. The Sage Handbook of Perfomance Studies. [www.sagepub.com](http://www.sagepub.com). (Imesomwa tarehe 20/03/2021)
- Wamitila, K.W. (2003). *Kamusi ya Fasihi, Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Publishers Ltd.
- Welch, E.A. (1974). *Life and Literature of the Sukuma in Tanzania East Africa*. Tasinifu ya Uzamivu. Howard University.
- Wilson, G. (1957). *The Land Rituals of Individuals among Nyakyusa*. Living Stone: The Phodes Living Stone Institute of Oxford.